JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# TAARIFA KWA UMMA

## DCEA YAKAMATA TANI 22.6 ZA DAWA ZA KULEVYA KATIKA OPERESHENI ZA MEI NA JUNI 2026.

**Dar es Salaam, 2 Julai, 2026:**
Katika kipindi cha mwezi Mei na Juni 2026, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ilifanya operesheni katika maeneo mbalimbali nchini na kufanikiwa kukamata tani 22.6 za dawa za kulevya, lita 30.5 na kilogramu 19.94 za dawa tiba zenye asili ya kulevya. Pia, iliteketeza ekari 228.5 za mashamba ya bangi pamoja na tani 3.3 za bangi na mirungi. Aidha, magari sita, bajaji mbili na pikipiki 33 zilikamatwa kuhusiana na uhalifu huo, huku watuhumiwa 188 wakikamatwa kwa hatua za kisheria.

Operesheni zilizofanyika jijini Dar es Salaam zilifanikisha ukamataji wa kilogramu 19.94 za bidhaa zilizotambulishwa kama virutubisho vya lishe aina ya AFA CELL (Moringa Extract) katika eneo la mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Baada ya kufanyiwa uchunguzi wa maabara, ilibainika kuwa bidhaa hizo zilikuwa na kiambata cha dawa tiba yenye asili ya kulevya aina ya Prazepam.

Bidhaa hizo ziliingizwa nchini kutoka Malaysia na zilikuwa zinaandaliwa kusafirishwa kwenda Barbados katika visiwa vya Karibiani. Kuhusiana na tukio hilo, watuhumiwa Agustino Metusela Ismaely (30), mkazi wa Kimara; Zamia Harid Upunda (23), mkazi wa Bungoni, Ilala; na Habiba Ally Mziga (54), mkazi wa Mbezi Makonde walikamatwa.

Prazepam ni dawa tiba yenye asili ya kulevya iliyopo katika kundi la *benzodiazepine* inayotumika kutibu magonjwa mbalimbali ikiwemo wasiwasi, msongo wa mawazo na kukosa usingizi. Endapo dawa hizi zitatumika kiholela au bila maelekezo ya daktari zinaweza kusababisha uraibu, kuharibu mfumo wa fahamu, mfumo wa upumuaji, kupoteza fahamu na hata kifo.

Katika operesheni nyingine iliyofanyika mtaa wa Manyanya, Kinondoni, zilikamatwa kilogramu 34.87 za mirungi iliyokuwa ikisafirishwa kwa kutumia gari aina ya Fuso lenye namba za usajili T 490 ECM kutoka Tarakea, mkoa wa Kilimanjaro. Mirungi hiyo iliyotokea nchini Kenya ilikuwa imefichwa kwa kuchanganywa na matenga ya nyanya ili kuficha uhalisia wa mzigo huo. Baada ya kufikishwa Dar es Salaam, ilishushwa katika eneo la kituo cha mafuta kilichopo mtaa huo kabla ya kuanza kusambazwa kwa kutumia usafiri wa bajaji yenye namba za usajili MC 361 CZV.

Katika tukio hilo, walikamatawa watuhumiwa Mohamed Omary Mohamed (24), utingo na mkazi wa Tandale; Suleman Omary Suguti (34), dereva wa gari hilo na mkazi wa Tarakea, Rombo; na Deo Paschal Maratua (32), dereva wa bajaji na mkazi wa Tandale kwa Mtogole. Aidha, mtuhumiwa Husseni Jumaa Salimu (52), mkazi wa Dar es Salaam, ambaye anadaiwa kuwepo Nairobi, Kenya, anatafutwa kuhusiana na tukio hilo.


08 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327, 11486 Dar es Salaam; Simu: +255 22 211 3754/57;
Nukushi: +255 22 211 3752; Barua pepe: cg@dcea.go.tz; Tovuti: www.dcea.go.tz

Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ulifanyika ukaguzi na uchunguzi wa bidhaa katika duka la bidhaa lijulikanalo kama *“village supermarket”* la jijini Dar es Salaam na kubaini uwepo wa vinywaji hususan “energy drinks” zenye viambata vya kemikali ya THC ambayo hupatikana kwenye dawa za kulevya aina ya bangi. Katika operesheni hiyo, jumla ya kopo 122 zenye ujazo wa mililita 250 kila moja, sawa na lita 30.5 zenye chapa ya “TRIP” zilikamatwa. Watuhumiwa Syed Abdul Bast (43) raia wa Pakistan na Dhirendra Kumar Gorodhan (45), mtanzania mwenye asili ya Asia walikamatwa katika tukio hilo.

THC ni kemikali inayopatikana kwenye dawa za kulevya aina ya bangi ambayo, ina madhara mbalimbali kwa mtumiaji ikiwemo, kuamsha magonjwa ya akili, kubadili utendaji kazi wa mfumo wa fahamu, kuchochea vitendo vya kihalifu ikiwemo wizi, unyang`anyi, ukatili na kuchochea matumizi ya dawa nyingine za kulevya.

Katika operesheni iliyofanyika eneo la ukaguzi wa mizigo la Bandari ndogo ya boti zinazotoa huduma kati ya Dar es Salaam na Zanzibar, zilikamatwa gramu 972.05 za mirungi zilizokuwa zikisafirishwa na mtuhumiwa Kalsam Abdurahman Sebbi (43), raia wa Kenya mwenye makazi yake Mombasa. Kadhalika wilayani Kigamboni zilikamatwa gramu 162.48 za heroin zilizomuhusisha mtuhumiwa Omary Miraji Mbonaeni.

Mkoani Arusha, zilikamatwa kilogramu 106.04 za dawa za kulevya aina ya mirungi zilizokuwa zikisafirishwa kwa kutumia gari aina ya Toyota Premio lenye namba za usajili T 853 ECX. Katika tukio hilo, alikamatwa mtuhumiwa Goodluck Erasto Nyakaselula (35), mkazi wa Mbezi Beach, Dar es Salaam, ambaye ni mtaalam wa picha za kitabibu (Radiographer) katika Hospitali ya Ocean Road ya jijini Dar es Salaam.

Aidha, wilayani Same mkoani Kilimanjaro, eneo la kituo cha mabasi yaendayo mikoani, zilikamatwa kilogramu 240 za mirungi zikiwa zimefichwa ndani ya mabegi ya nguo. Katika tukio hilo, walikamatwa watuhumiwa Irene Obedi Sule na Eliasi Obedi Sule.

Kufuatia operesheni zilizofanyika katika mikoa mingine nchini, zilikamatwa tani 19.5 za bangi, tani 2.6 za mirungi, gramu *11.63* za heroin na kilogramu 40 za skanka. Aidha, tani 3.3 za bangi na mirungi pamoja na ekari 228.5 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika wilaya za Chamwino mkoa wa Dodoma, kijiji cha Mwengei kilichopo wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi na katika vijiji vya Busekeseke na Miembeni vilivyopo wilaya ya Sengerema na Geita.

Kupitia ushirikiano wa kiutendaji kati ya Tanzania na nchi za Eswatini, Afrika Kusini, Msumbiji na Zambia, imebainika kuwepo kwa wahalifu wa mitandao ya biashara ya dawa za kulevya ambao ni raia wa Tanzania waliokimbilia kwenye nchi hizo. Kufuatia taarifa hizo, DCEA kwa kushirikiana na mamlaka husika za nchi hizo itaendelea kufanya operesheni za pamoja kwa lengo la kuwakamata na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria.

Vilevile, Kwa kushirikiana na Mamlaka za udhibiti DCEA imeweka mikakati ya kukabiliana na usafirishaji wa dawa za kulevya kupitia virutubisho vya chakula, dawa na kemikali kwa kubadilishana taarifa, kufanya kaguzi na operesheni za pamoja ili kulinda afya na ustawi wa jamii.

Imetolewa na;

Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA**
**NA DAWA ZA KULEVYA.**


08 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327, 11486 Dar es Salaam; Simu: +255 22 211 3754/57;
Nukushi: +255 22 211 3752; Barua pepe: cg@dcea.go.tz; Tovuti: www.dcea.go.tz